Teacher.co.ke

# KISWAHILI FORM 3

# MARKING SCHEME

# TERM 1 OPENER EXAM 2022

INSHA

Andika ratiba kuhusu siku ya kutuza wanafunzi bora shuleni.

1. UFAHAMU (ALAMA 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata

Uwezo wa mtu kudanganya huonekana mapema zaidi na katika dunia yenye watu wakazi tofauti uwezo huu huonekana katika kila aina ya watu duniani kwa kipindi cha mapema zaidi.

Saikolojia ya nadharia ya uwongo ambapo mtu anaweza au kuufinyanga anavyotaka nikidi ambapo mtu ana miaka minne, lakini si nchini ya hapo.

Watoto hujifunza kutokana na uzoefu na kama wakigudua kwamba wanaposema uwongo wanaadhibiwa huacha kusema uwongo mpaka pale ambapo wanajua namna ya kuunga uwongo wao na kuacha maswali ambayo hayawezi kujibika.

Watoto wanapokuwa wameshajua namna ya kuujenga uwongo mpaka ukakubalika wanakuwa hatari zaidi kwani wanakuwa wameshatoka katika maadili ya kawaida ya ubaya wa kudanganya.

Watoto hawa huweza kujifunza kudanganya baada ya kuona kwa miaka mingi watu wanavyodanganya. Wengine hudanganya kwa bahati mbaya na wengine huwa na tabia mbaya.

Wanaodanganya kwa bahati mbaya mara nyingi hubadilika wanapokuwa watu wazima, lakini pia hata wale wanatengeneza tabia hubadilika baadaye lakini si sana.

Wakati fulani wapo watu wanaofikiri kwamba watoto hudanganya zaidi kuliko watu wazima.

Uwongo wa watu wazima huwa mbaya zaidi na wenye utata mkubwa kuutambua na hii hutegemea zaidi mbinu za udanganyifu, mazingira na tabia nyingine za watu wazima. Na wapo watu wazima wenye tabia ya kudanganya au kwa lugha ya kitaalamu, pseudolojia fantastika.

Wanafalsafa kama Mtakatifu Augustine, na pia Thomas Aquinas na Immanuel Kant, wanalaani aina zote za udanganyifu. Kwa mujibu wa watu hao watatu hakuna sababu ya aina yoyote ile ya kudanganya.

Ni vyema mtu akauawa, kuteseka au kupata magumu kuliko kudanganya hata kama njia moja pekee iliyobaki ya kujihami ikiwa ni hiyo. Wanafalsafa hao wanasema kwamba kudanganya kunaharibu uwezo wa mtu kuaminika katika jamii au jamii yenyewe kuaminika.

a) Ipe taarifa anwani mwafaka. (alama 2)

- Udanganyifu wa mwanadamu.
- Namna mtoto anavyojenga udanganyifu. / Uwongo

b) Ni katika hali gani uwezo wa mtu kudanganya huonekana mapema zaidi? (alama 2)

- Katika dunia ya watu wa kazi tofauti na katika kila aina ya watu duniani



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

c) Ni wakati gani uwongo waweza kuwa hatar[illegible]i. (alama 2)

- Wakati mtoto atakuwa ameshatoka katika maadili ya kawaida ya ubaya wa kudanganya

d) Ni nini sababu ya watoto kudanganya. (alama 3)

i) Baada ya kuona kwa miaka mingi watu wanavyodanganya.
ii) Wengine ni kwa bahati mbaya.
iii) Wengine huwa na tabia mbaya

e) i) Eleza mtazamo wa mtakatifu Augustine na Thomas Aquinas kuhusu udanganyifu. (alama 2)

- Kuwa hakuna sababu ya aina yoyote ile ya mtu kudanganya.

ii) Kulingana na watu waliotajwa hapo juu kudanganya kuna madhara gani. (alama 2)

- Kunaharibu uwezo wa mtu kuaminika katika jamii au jamii yenyewe kuaminika.

f) Eleza maana ya msamiati kama ulivyotumika katika taarifa. (alama 2)

i) Kuufinyanga – Kubuni / Kujenga uwongo

ii) Kujihami – Kujichunga nafsi usidhurike / Kujitetea usijipate kwa matatizo / Kujitetea ili ujiondoe kwa matatizo

## 2. MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 25)

a) Andika sauti yenye sifa zifuatazo.

i) Sauti ya kaa kaa laini. (alama 1)

/k/, /g/, /ng'/, /gh/

ii) Kikwamizo cha ufizi. (alama 1)

/s/ /z/

b) Tofautisha maana ya sentensi zifuatazo. (alama 2)

i) Maziwa yote yamemwagika

Kwa ujumla / bila kubakisha

ii) Maziwa yoyote yatamfaa mtoto

Bila kuchagua / kutojali

c) Eleza maana ya mofimu. (alama 2)

Sehemu ndogo ya neno inayowasilisha maana.

d) Andika ukubwa wingi wa. (alama 2)

Mwizi aliiba kikapu na ng'ombe.

Majizi yaliiba majikapu na magombe.

e) Yakinisha kwa umoja. (alama 2)

Kamba zisingekatika zisingepotea.

Kamba ingekatika ingepotea.

f) Andika kwa usemi wa taarifa. (alama 3)

"Viungo hivi havitatosha kuunga mchuzi wenu," mpishi alilalamika.

Mpishi alilalamika kuwa viungo hivyo havingetosha kuunga mchuzi wao.

g) Tunga sentensi mbili kuonyesha maana tofauti za neno 'jua' (alama 2)

i) Jua huchomoza asubuhi na hutua jioni.

ii) Baba alipoitwa shuleni, alijua kulikuwa na jambo baya

(Mwalimu akadirie majibu ya mwanafunzi)

h) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo. (alama 2)

i) Tuma – mtumwa, utumwa, mtume

ii) Lima – kilimo, mkulima, ukulima

(nomino moja ✓ 1)



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes
For more FREE KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/

Teacher.co.ke

i) Eleza tofauti ya sentensi zifuatazo. (alama 2)

(i) Ningefurahi kama ungefanya kazi.

Kuna uwezekano

(ii) Ningalifurahi kama ungalifanya kazi.

Hakuna uwezekano

j) Kanusha sentensi ifuatayo (alama 2)

(i) Mkiondoka mapema mtafika kwa wakati.

Msipoondoka mapema hamtafika kwa wakati

k) Jaza pengo. (alama 2)

| kitenda | kitendeshwa | kitendeshea |
|---|---|---|
| Lia | Lizwa | Lizia |
| Cheza | chezeshwa | chezeshea |

(4 X ½ = 2)

l) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi ya kistari kifupi. (alama 2)

i) Tarehe → Wageni watawasili tarehe 2-01-2022.

ii) Ufafanuzi wa maelezo. Mboni ya jicho – sehemu ya ndani ya jicho.

(Mwalimu akadirie majibu ya mwanafunzi)

ISIMU JAMII (ALAMA 5)

A: Wee kuja hapa! Wewe ni nani? Sema haraka !

B : Mimi ….. ni….. afande Lona.

A : Unatoka wapi saa ii?

a) Tambua sajili hii. (alama 1)

Sajili ya polisi/askari washika doria

b) Fafanua sifa za sajili hii. (alama 4)

- Lugha hutumia msamiati maalum. mf Afande
- Lugha huwa na utohozi. mf. Twende stesheni
- Lugha ni ya kuamrisha – Kuja hapa!
- Lugha si sanifu mf. Unatoka wapi saa ii?
- Lugha huchanganya ndimi
- Lugha ya udadisi/maswali – wewe ni nani? Unatoka wapi?

(4 X 1) = 4

FASIHI SIMULIZI (ALAMA 5)

Fafanua umuhimu wa nyimbo katika jamii.

i) Nyimbo huburudisha jamii
ii) Hutoa mafunzo kwa jamii/kuelimisha
iii) Huhifadhi utamaduni wa jamii
iv) Hutumiwa kupitisha ujumbe muhimu.
v) Hufunza maadili
vi) Hukashifu tabia zisizokubalika
vii) Huliwaza k.m mbolezi
viii) Ni kitega uchumi kwa baadhi ya wasanii wa muziki (5 X 1) = 5



Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

For more FREE KCSE Mocks, Notes, Exams, and Past Papers Visit https://Teacher.co.ke/notes/